

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA TATU

YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA NANE

12 MEI, 2016

MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA NANE

TAREHE 12 MEI, 2016

I. DUA:

Saa 3.00 asubuhi Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

Makatibu Mezani

1. Ndg. Joshua Chamwela
2. Ndg. Neema Msangi

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani.

1. Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo aliwasilisha Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
2. Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Tathmini ya Utendaji wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2014/15 (*The Annual Performance Evaluation Report of The Public Procurement Regulatory Authority for the Financial Year 2014/2015*).

TANGAZO:

Spika aliwatangazia Wabunge kutokuwepo kwa Waziri Mkuu na hivyo Maswali ya Waziri Mkuu hayatakuwepo.

III. MASWALI YA KAWAIDA:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge;

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na.150 – Mhe. Ritta Enespher Kabati (kny. Mhe. Maida Hamad Abdallah)

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Ritta Enespher Kabati

(ii) Mhe. Mary Pius Chatanda

(iii) Mhe. Cecilia Daniel Paresso

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Swali Na.151 – Mhe. Joel Mwaka Makanyaga

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Joel Mwaka Makanyaga

(ii) Mhe. Raphael Japhary Michael

(iii) Mhe. Juma Selemani Nkamia

Swali Na.152 – Mhe. Ali Salim Salim Khamis

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Ali Salim Khamis

(ii) Mhe. Richard Mganga Ndassa

(iii) Mhe. Daniel Nsanzugwanko

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

Swali Na.153 – Mhe. Mwitwa Mwikwabe Waitara

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Mwitwa Mwikwabe Waitara

(ii) Mhe. Suzan Anselm Lyimo

(iii) Mhe. Bonnah Moses Kaluwa

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Swali Na.154 – Mhe. Faida Mohamed Bakar

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Faida Mohamed Bakar

(ii) Mhe. Raisa Abdalla Mussa

IV. MATANGAZO:

1. Wageni wote waliokuwepo Bungeni walitambulishwa;
2. Mhe. Andrew Chenge – Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo aliwatangazia Wajumbe wake wakutane ukumbi Na. 227 saa 7.00 mchana;
3. Mhe. Balozi Adadi Rajab – Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama aliwatangazia wajumbe wake wakutane ukumbi Na. 227 saa 7.00 mchana;
4. Mhe. Dkt. Norman Adamson Sigalla King – Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu aliwatangazia Wabunge wa kamati hiyo kukutana Hazina saa 7.00 mchana;
5. Mhe. Atashasta Justus Nditiye - Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii aliwatangazia Wajumbe wake kukutana saa 7.00 katika Ukumbi wa Msekwa “C”;
6. Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini aliwatangazia Wajumbe wake wakutane katika Ukumbi wa Msekwa saa 7.00 mchana.

UAMUZI WA SPIKA JUU YA HOJA/MWONGOZO JUU YA MAGARI YA WASHAWASHA:

Spika, alitoa nafasi kwa Mhe. Suzan Anselm Lyimo ili afute kauli yake au athibitishie juu ya ununuzi wa magari 777 ya washawasha yaliyonunuliwa na Serikali Mwaka 2015, kama ilivyokuwa imeelezwa kwenye Mwongozo ulioombwa awali na yeye Mhe. Suzan Lyimo.

Mhe. Susan Lyimo alisisitiza kuwa Hoja yake ni ya kweli kwa ushahidi wa Jamii Forum na *Hansard* ya tarehe 4/2/2016 na 20/10/2015 pamoja na kuonesha swali la nyongeza alilouliza Mhe. Suzan kwa swali la Mhe. Juma Selemani Nkamia na Waziri akasema katika majibu yake kuwa sio magari hayo tu bali yataongezwa mengine.

Mhe. Spika alitoa maelekezo kwa Mhe. Suzan Anselm Lyimo aandike vizuri ushahidi huo kisha apeleke kwa Ofisi ya Spika ili uende katika Kamati ya Maadili.

MWONGOZO WA SPIKA:

1) Mhe. Anatropia Theonest Lwehikila alitumia Kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo pamoja na Kanuni ya 46 kuhusu kujibu swali kwa ukamilifu, kwamba wakati Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano akijibu swali namba 152, kwenye swali dogo la nyongeza la Mhe. Richard Ndassa, alipouliza bei ya nauli (ndege) hupangwa na nani, Naibu Waziri alijibu ni soko. Hivyo majibu hayaridhishi kwani bei za *Fast Jet* hupanda kiholela.

Spika alimwomba Mhe. Anatropia Lwehikila asome Kanuni na kuona namna bora ya kuleta Hoja yake Bungeni.

2) Mhe. Jopeph Osmund Mbilinyi alisimama kwa Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo kuwa Wizara ya Afya inahusika na Hospitali za Rufaa kama Muhimbili na Bugando, lakini Hospitali ya Bugando ina friji haba katika *mortuary* yake na zinazofanya kazi ni sita tu.

Spika alisema, mara nyingi Wabunge huomba kuchangia lakini bado hawaelewi kinachotakiwa kuchangiwa kwani Waziri wa Afya hahusiki na vitu kama Ambulance wala Zahanati; hata Wizara ya Elimu haihusiki na baadhi ya masuala ya Elimu ni TAMISEMI ndio imebeba mzigo mkubwa. Hivyo alimjibu Mhe. Mbilinyi kuwa atampa nafasi ya kuchangia.

- 3) Mhe. Kasuku Samson Bilago aliomba Mwongozo kwa kanuni ya 68(7) kwamba Miongozo imekuwa haipati majibu. Kwa mfano, upo mwongozo juu ya namna ya Waheshimiwa Wabunge kusaini Bungeni kama wataendelea kusaini mara mbili au moja?

Spika, aliahidi kujibu kabla ya saa 7.00 mchana leo.

V. HOJA ZA SERIKALI:

- Hoja ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Uchangiaji uliendelea kama ifuatavyo:-

- | | | |
|--------------------------------|---|-----|
| 33) Mhe. Rashid Ali Abdallah | - | CUF |
| 34) Mhe. Taska Restituta Mbogo | - | CCM |

TANGAZO:

- Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Mhe. Mwigulu Nchemba aliwaomba Wabunge Wafugaji wa Mikoa ya Simiyu na Mara waonane.
- Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo – Wageni wake kutoka South Africa (kundi la Mafikizoro ambao ni Ndg. Motlantia Chiza, Ndg. Thiodore na Ndg. Modise Gomo) wakiwa na Mwenyeji wao Ndg. Nassib Abdul Juma (Diamond) aliyeambatana na Ndg. Salan Sherafi, Ndg. Hamis Aletale na Ndg. Kamba Ashraf.

Uchangiaji uliendelea kama ifuatavyo:-

- | | | |
|-----------------------------------|---|---------|
| 35) Mhe. Edward Franz Mwalongo | - | CCM |
| 36) Mhe. Suzana Mgonokulima | - | CHADEMA |
| 37) Mhe. Bonnah Moses Kaluwa | - | CCM |
| 38) Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi | - | CHADEMA |
| 39) Mhe. Najma Murtaza Giga | - | CCM |
| 40) Mhe. Hussein Mohamed Bashe | - | CCM |
| 41) Mhe. Ester Amos Bulaya | - | CHADEMA |
| 42) Mhe. Rashid Mohammed Bakar | - | CCM |
| 43) Mhe. Faida Mohammed Bakar | - | CCM |
| 44) Mhe. Ruth Hiyob Mollel | - | CHADEMA |
| 45) Mhe. Fredy Atupele Mwakibete | - | CCM |
| 46) Mhe. Salma Mohamed Mwassa | - | CUF |
| 47) Mhe. Seif Khamis Said Gulamal | - | CCM |

MATANGAZO:

Mhe. Nape Moses Nnauye alitangaza kuwa kutakuwa na Onesho UDOM leo na kesho atakuwepo Mwimbaji King Kikii kesho jioni katika viwanja vya Bunge.

Kuhusu Waheshimiwa Wabunge kusaini system ni ya *kupress & hold* na ni mara mbili asubuhi na jioni.

VI. KUSITISHA BUNGE:

Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni.

VII. BUNGE KUREJEA:

- Saa 10.00 Bunge lilirejea na kuongozwa na Mwenyekiti, Mhe. Mussa Azzan Zungu. Majadiliano yaliendelea kwa wafuatao:-

- 48) Mhe. Kabwe Ruyagwa Zitto - ACT
- 49) Mhe. Kemilembe Julius Lwota - CCM
- 50) Mhe. Riziki Shahari Mngwali - CUF
- 51) Mhe. Flatei Gregory Massay - CCM
- 52) Mhe. Maria Ndila Kangoye - CCM
- 53) Mhe. Joseph George Kakunde - CCM
- 54) Mhe. Innocent Sebba Bilakwate - CCM
- 55) Mhe. Dkt. Elly Marco Macha - CHADEMA
- 56) Mhe. Daimu Iddy Mpakate - CCM
- 57) Mhe. Dua William Nkurua - CCM
- 58) Mhe. Joram Ismael Hongoli - CCM
- 59) Mhe. Kasuku Samson Bilago - CHADEMA
- 60) Mhe. Felista Aloyce Bura - CCM
- 61) Mhe. Azza Hilal Hamad - CCM
- 62) Mhe. Margareth Simwanza Sitta - CCM
- 63) Mhe. Mussa Rashid Ntimizi - CCM
- 64) Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu (Mhe. Dkt. Abdallah Possi).
- 65) Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora (Mhe. Selemani Said Jafo)
- 66) Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora (Mhe. Angellah Jasmine Kairuki).
- 67) Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Mhe. George Mcheche Masaju)

VIII. KAMATI YA MATUMIZI:

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi na kupitisha Vifungu vyote vya Wizara hii bila marekebisho.

IX. KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 2.24 Usiku Bunge liliahirishwa hadi tarehe 13/5/2016 siku ya Ijumaa saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA
12 MEI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**